



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UJENZI WA OFISI ZA TUME JIJINI DODOMA**

**UNAENDELEA KUKAMILIKA**

**Dodoma, 07 Januari 2020.**

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahera Charles amesisitiza kwamba Tume itahamia Dodoma mwaka huu (2020).

Dkt. Mahera ameyasema hayo jana (tarehe 06.01.2020) mara baada ya kufanya ziara kwenye eneo la Njedengwa, Jijini Dodoma zinapojengwa ofisi za Tume na kujionea maendeleo ya ujenzi ambao unafanywa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT).

“Mwaka huu wa 2020 ni mwaka wa uchaguzi, mambo yote yatafanyikia hapa Dodoma,” amesema Dkt. Mahera.

Mkurugenzi huyo ambaye aliambatana na Mwenyekiti wa Tume, Mhe. Jaji Rufaa (mst) Semistocles Kaijage amesema kwamba JKT ambao walikabidhiwa mradi huo baada ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kushindwa kukamilisha mradi kwa wakati ulopangwa, wameihakikishia Tume kwamba mradi huo utakamilika ifikapo mwenzi Aprili mwaka huu.

“Mkandarasi wa kwanza alikuwa TBA, baada ya kuwa ameondolewa imetuchukua kama mwenzi mzima kuweka utaratibu wa kuandaa michoro upya kwa sababu michoro ilikuwa imekosewa sana. Kwa ushirikiano wa Ardhi Univesity (Chuo cha Ardhi) na SUMAJKT kazi imeanza na inaenda kwa kasi kubwa,” amesema Dkt. Mahera.

Dkt. Mahera amesema kwamba SUMAJKT imeweka vijana zaidi ya mia tatu (300) kwenye eneo hilo la ujenzi na kwamba Tume tayari imelipatia Shirika hilo malipo ya awali (advance payment) kwa ajili ya kazi hiyo.

“Sisi tumeshawapatia advance payment (malipo ya awali) na kazi imeanza kwa kasi kubwa, kwa pamoja majengo yote matatu yaani ghala, jengo la kutangazia matokeo na ofisi hii yenye floor (ghorofa) nane vyote vitaendelea kwa wakati mmoja,” amesema.

Mkurugenzi Mahera amesema kwamba Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Brigedia Jenerali Charles Mbuge amemhakikishia kwamba itakapofika mwezi Aprili mwaka huu mradi huo utakuwa umefikia hatua nzuri sana.

“Bahati nzuri Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Brigedia Jenerali Charles Mbuge alikuwa hapa juzi Jumamosi, alikuja kukagua vijana wake na ameniahidi kwamba itakapofika Aprili mwaka huu tutakuwa tupo mbali sana, na mimi naahidi kwamba Tume itatoa ushirikiano wa hali ya juu sana kwa SUMAJKT,” alisema.

Kwa upande wake, Lazaro Masanja ambaye ni Mhandisi Miradi wa SUMAJKT amesema kwamba nguvu kazi ya vijana 300 iliyowekwa na Jeshi hilo kwenye mradi huo inaashiria kwamba Jeshi lipo makini kuhakikisha kwamba mradi unakamilika mapema iwezekanavyo.

“Kama ilivyo kauli mbiu ya Mkuu wa JKT *‘Jeshi Halishindwi’*, kwa hiyo sisi matarajio yetu ni kwamba mwezi wa nne tutakuwa aidha tumekabidhi au tuko kwenye maandalizi ya kukabidhi kazi hii,” alisema.

Katika hatua nyingine, Mhandisi huyo ameushauri Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya marekebisho ya kalavati ambalo limejengwa karibu na eneo la mradi wa Tume ambalo wakati wa mvua linatiririsha maji mengi kuelekea kwenye moja ya majengo ya mradi huo.

Imetolewa na:

**Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura**